MTIHANI WA ZIADA KIDATO CHA KWANZA

MASWALI YA KUDURUSU 2019/2020

KIDATO CHA 1 KISWAHILI KARATASI YA 1,2 NA 3
MTIHANI 1-10

MTIHANI 1

SEHEMU A: UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Jukwaani chini kulia kuna mlango wa kutokea. Linapofunguka pazia, Mama Tatu anaonekana akisuka ukili. Anaelekea mlango wa kutokea nje. Mlango wa kuingilia ndani upo upande wake wa kulia.

Mama: *(Anamtazama bila kupendezewa). Anasema huku anasuka ukili)* Hmm. Hiyo kanzu imezidi tena. Si unatembea uchi hivyo. Fupi, fupi, imekubana. Ndio uambiwe nini? Mzungu sana!

Tatu: Mama, watoto wote wanavaa hivi hivi siku hizi *(Ananung'unika).*

Mama: Hm. Haya sisi yetu macho tu. Maana husikizi tena. Umekuwa mkubwa, siwezi kukupiga. Basi haya fanya utakavyo tu. *(Kimya).*

Tatu: Maa. *(Kwa hofu kidogo).*

Mama: Sema tu, nakusikia.

Tatu: (Ahema) Nataka ruhusa kwenda sinema.

Mama: Sinema gani?

Tatu: Empress.

Mama: Basi si bado? Leo ndio kwanza Ijumaa, "Lady Show" Jumapili.

Tatu: Nataka kwenda leo usiku.

Mama: Toka lini ukaenda sinema usiku? Siku zote unakwenda Jumapili mchana. Mchana sikukatazi, lakini usiku hapana, hapana, hata kidogo. Kwanza pesa za kukupa wewe kila Jumapili ziko wapi? Baba yako hali yake unaijua. Kila siku hapa analalamika kodi zimekuwa nyingi. Nawe unamsikia. Kodi ya kichwa, kodi ya miguu, kodi ya uzee, kodi ya mapato, kodi ya wafanyakazi, kodi, kodi, iiee! Nawe unataka sinema. Pesa zenyewe ziko wapi?

Tatu: Mie sitaki pesa mama, nipe ruhusa tu. Swai atanichukua sinema. *(Ma Tatu ameshtuka.Anamtazama Tatu. Anarudia kusuka ukili wake).*
(kimya)

Tatu: Ma, atakuja sasa hivi. Jee nende? (kimya).

Mama: (Polepole) Na huyu Swai ndio nani?

Tatu: Mtoto mmoja Swai Hamisi. Najuana naye.

Mama: Mwanamume?

Tatu: (Anaitika kwa kichwa).

Mama: Nae anakuchukua sinema – Na kwa nini yeye akulipie sinema? Anakujuaje? Baba yako? Au nani? *(Anaacha kusuka)*
(Kimya).

Mama: *(kwa sauti ya juu)* Nijibu! Wewe unafikiri, anapata taabu hii yote ya kukuchukua sinema kwa nini, eh? Wewe mwana mzima sasa huwezi kufikiria?

Tatu: Mama ingekuwa kuna jambo lolote baya tusingetaka ruhusa. Swai ni rafiki tu.

Mama: Hakuna urafiki baina ya mtoto wa kiume na mwanamwali hata kidogo. Uwongo. Usitudanganye. Hivi unaniona mjinga sana, eh?

Tatu: Mama *(kwa sauti ya kubembeleza)* siku hizi watoto wote wanakwenda na marafiki wa kiume

kutembea, si kitu geni.

Mama: Sio uzungu! Ndio kuiga uzungu tena. Basi sisi si wazungu. Mzungu na Mwafrika mbalimbali. Mila zetu mbalimbali. Wao hawana haya, anaweza kwenda na mume huyu na mume yule isiwe kitu.

(Ebrahim Hussein, Michezo ya Kuigiza, Nbi: EAPH, 1980)

Kwa majibu ya maswali haya piga simu ama utume ujumbe kwa BWANA CHEPKWONY COSMAS 0724351706 upate usaidizi

MASWALI

1. Pendekeza kichwa mwafaka kwa kifungu hiki. (alama 1)

2. Taja wahusika **wawili** wa kiume waliorejelewa katika kifungu hiki. (alama 2)

3. Taja sababu **nne** zilizomfanya Mama amzuie Tatu kwenda sinema. (alama 4)

4. Eleza tofauti kati ya mila za Wazungu na za Waafrika asilia kulingana na kifungu hiki. (alama 3)

5. Huku ukitolea mifano kutoka kwenye kifungu, onyesha tabia **tatu** za Tatu. (alama 3)

6. Ina maana gani kusema "Haya sisi yetu macho tu"? (alama 2)

SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 15)

1. Toa mfano mmoja mmoja kwa kila aina ya konsonanti uliyopewa. (alama 2)

   (i) Kipasuo: _____

   (ii) Kitambaza:_____

2. (a) Taja vipashio vya lugha. (alama 2)

   (b) Rekebisha sentensi hii: Mwalimu ambaye aliyenifunza amekuja. (alama 2)

   _____

3. Bainisha viambishi awali, mzizi na viambishi tamati katika maneno yafuatao: (alama 3)

	Viambishi awali	Mzizi	Viambishi tamati
Atakutengenezea			
Wasaidieni			

4 Andika sentensi zifuatazo katika ukubwa.

(i) Wanawake hao waliuza mbuzi wao wote. (alama 1)

(ii) Kigari chake kiliharibikia katika kibonde chenye kijito. (alama 2)

5 Tunga sentensi kuonyesha tofauti ya ki maana kati ya maneno haya. (alama 2)

(a) Vua:_____

(b) Fua:_____

6 Utatafuta maneno gani kwenye kamusi, ukitaka kujua maana za maneno yafuatayo. (alama 1)

(a) Kucheza: _____

(a) Usinipige:_____

SEHEMU C: USHAIRI (ALAMA 10)

Wapenda mtu kwa kitu

Shairi nakuleteya, tafadhali mwana twaa
Hikwita hunikimbiya, na kunitiya tama
Kumbe mebadili niya, hata washenzi watwaa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Nilidhani u libasi, njema ya mtu kuvaa
Hawa sina wasiwasi, popote ninapokaa
Kumbe u mtu rakhisi, atakaye hukutwaa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Usinionye mija, miuja haitafaa
Kwamba huna nami haja, ukinambia si baa
Mtu hupenda kimoja, sende nami kwa hadaa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Umejifunza wekevu, kutaka kunihadaa
Na huno wako uovu, ni bure hautafaa
Mimi ni wana mtuvu, sitendwi hataataa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Kunena mangi nataka, lakini wasaa
Na hapa tulipofika, ni kheri hakuambaa
Maana u mtu nyoka, huna ahadi u baa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Tamati sineni sana, muhibu toa tamaa
Ulotenda nishaona, wala hutanihadaa
Sasa kheri kuatana, kulla mtu akaa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.
(Kutoka, Malenga wa Mvita, uk. 163)

Maswali

1. Shairi la mishororo minne katika kila ubeti huitwa? (alama 1)
2. Tambua vina katika ubeti wa pili. (alama 2)
3. Eleza maana ya 'Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu,' alama 2)
4. Taja mambo **matatu** ambayo msemaji analalamikia katika shairi? (alama 3)
5. Maneno yafuatayo yameendelezwa kishairi. Yaandike kwa njia sanifu: (alama 2)
   (a) hikwita: _____
   (b) kuatana: _____

SEHEMU D: ISIMUJAMII (al.4)

(a) Isimu jamii ni nini? (alama 2)

Eleza mambo **mawili** anayozingatia mzungumzaji yeyote ili kutumia lugha inavyofaa. (alama 2

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 6)

(i) Kuna tofauti gani kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama
(ii) Eleza tofauti **mbili** kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama 2)
(iii) Eleza tofauti kati ya: (alama 2)

(a) Hekaya: _____

(b) Hurafa _____

Kwa majibu ya maswali haya piga simu ama utume ujumbe kwa

BWANA CHEPKWONY COSMAS 0724351706 upate usaidizi

MTIHANI 2

SEHEMU YA A: INSHA . (ALAMA 20)
Fafanua namna ajali za barabarani zinaweza kuzuiwa nchini Kenya.

SEHEMU B: SHAIRI (ALAMA 15)
Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali.
Kila mdharau chake

Kuzimu wenda kuona, kila mdharau chake
Cha kwake akikana, kutumai cha mwenzake
Fahamu anayo laana, mpiga chake mateke
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Siringe na kujivuna, chako ukakipa teke
Unavunja lako jina, ili watu wakucheke
ana laana kwa Rabana, kila mdharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Awe Fatu na Amina, au Asha ndugu yake
Katu hawatafanana, kila mtu hadi yake,
Kila mjuzi wa mana, huwa hadharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Tama naomba amina, kilicho chetu tushike
Kidumu na kulingana, na tukipe hadhi yake
Ana laana kwa Rabana, kila mdharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

(*Diwani ya Akilimali na Akilimali Snow-White, K.L.B*)

Maswali:
1. Elezea ujumbe unaojitokeza katika ushairi huu. (al 2)
2. Nakili kibwagizo cha ushairi huu. (al 1)
3. Elezea aina za ushairi huu kwa kuzingatia: (al 6)

i. mishororo
ii. vina
iii. vipande

4. Elezea mambo matatu ambayo mshairi anatuonya dhidi yake. (al 3)
5. Elezea maana ya maneno haya: (al 3)
    a. siringe
    b. katu

c. hadhi

SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a. Elezea tofauti kati ya sauti /d / na / z/ (al 2)

b. Onyesha silabi inayowekwa shadda katika maneneo haya. (al 3)

i. umio
ii. kinywa
iii. mmomonyoko

c. Tunga sentensi moja ukitumia nomino ya kitenzi jina. (al 2)

d. Andika sentensi ifuatayo kwa wastani. (al 2)

Magoma hayo yatachezwa mawanjani.

e. Tambua viambishi awali na tamati katika neno: (al 3)

Achezaye

f. Taja vipashio vya lugha kisha utolee mfano kwa kila kipashio: (al 4)

g. Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari. (al 2)

Naam, amekula kichache

Jaza pengo kwa kutumia kinyume sahihi cha kitenzi kilichopigiwa mstari. (al 2)

i. Mimi nilim---------- kunguru aliyokuwa amenaswa.
ii. Alivaa sare asubuhi kisha ---------- jioni

h. Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno: chuo (al 2)

i. Onyesha KN na KT katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mpishi yule hodari atatuzwa vizuri sana.

j. Tunga sentensi **tatu** kudhihirisha matumizi mawili tofauti ya kibainishi. (al 3)

k. Elezea maana ya kiimbo (al 2)

l. Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (al 2)

Hao wenyewe hawakusomea mafunzo ya ukulima bora.

m. Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kielezi . (al 2)

n. Bainisha ngeli za majina haya. (al 3)

i. zeruzeru
ii. ugwe
iii. saa

o. Yakinisha: Hukuja kunitembelea kazini. (al 2)

p. Kamilisha methali: (al 2)

Maiti haulizwi

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

i. Taja vipera vine vya semi. (al 4)

ii. Eleze:

A .Sifa za semi (al 4)

B.Umuhimu wa semi (ala4)

iii. Elezea maana ya nahau hizi. (al 2)

a. kukunja jamvi ----------

b. kupata jiko ----------

iv. Fanani ni nani katika fasihi simulizi? (al 1)

SEHEMU E: ISIMU JAMII

Elezea sifa **tano** za sajili ya hospitalini.

MTIHANI 3

2.USHAIRI

SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI YATAKAYOFUATA

Maisha siko imara, nakumbuka yako sura,
Ee kwangu ni kisura, usoni sitakukera,
Wangu kuja kwangu bara, u kamwe kwenye fikira.
Ukipendwa wewe penda, mapenzi ni kujienzi.

Banati nakuhitaji, kila siku kama maji,
Mbona chengoni hauji, hulipendi letu jiji,
Huenda sina kipaji, nitapata wapi taji?
Ukipendwa nawe penda, mapenzi ni kijienzi.

Mimi sasa nakuenzi, kwangu wewe ni kimanzi,
Kidosho nipe mapenzi, nisije funga kitanzi,
Mapenzi sivyo vihunzi, usiruke kama panzi,
Ukipendwa nawe penda, mapenzi ni kujienzi.

Mwenzangu nakuthamini, bali we huniamini,
Mseja napiga honi, moyoni sina amani,
Siipendi mitihani, sisite fanya hisani,
Ukipendwa nawe penda, mapenzi ni kujienzi.

Nitasema mara kenda, kuwa mimi nakupenda,
Maneno haya si ganda, kidole tapata shada,
Usoni nikikulinda, furaha tele tatanda,
Ukipendwa nawe penda, mapenzi ni kujienzi.

Nikwonapo napagawa, sasa nitoe ukiwa,
Mwenzako nina kipawa, nitakupa kama kawa,
Tutapata zetu mbawa, na kuishi kama njiwa,
Ukipendwa nawe penda, mapenzi ni kujienzi .

MASWALI

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)

(b) Taja aina ya shairi hili na utoe sababu. (alama 2)

(C) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 3)

(d) Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili na utoe mifano.(alama 2)

(e) Taja mbinu mbili za uhuru wa mshairi zilizotumika katika shairi hili na utoe mifano. (alama 2)

(f) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(g)Andika hoja nne kudhihirisha kwamba hili ni shairi la arudhi. (alama 2)

3.FASIHI

(a) Fasihi ni nini? (alama 1)

(b) Taja aina za fasihi na utoe ufafanuzi. (alama 2)

(c) Eleza dhima **tano** za fasihi. (alama 5)...

(d) Eleza sifa **tano** za mtambaji bora. (alama 5)

(e) Eleza tofauti **tano** kati ya aina za fasihi ulizotaja katika swali la (b). (alama 5)

(f) Taja makundi ya fasihi andishi. (alama 2)

4.MATUMIZI YA LUGHA

(a)(i) Taja sauti mbili za lugha ya Kiswahili na utoe mifano. (alama 2)

(ii) Taja aina mbili za ala za kutamkia na utoe mfano mmoja mmoja. (alama 2)

(iii) Linganisha sauti /e/ na /i/. (alama 2)

(iv) Tofautisha sauti /w/ na /b/. (alama 1)

(b)(i) Eleza maana ya silabi. (alama 1)

(ii) Onyesha silabi katika neno hili na ueleze aina ya kila moja. **Daftari** (alama 2)

(iii) Taja miundo miwili ya silabi za Kiswahili na utoe mifano. (alama 2)

(c)(i) Eleza maana ya kiimbo. (alama 1)

(ii) Onyesha shadda katika maneno haya. (alama 1)

mwana

seremala

(d) Yakinisha sentensi hii. (alama 1)

Nisipomlipa leo hataweza kusafiri.

(e) Andika sentensi hii katika hali ya mazoea. (alama 1) Mtoto ambaye alilia ni wetu.

(f) Kanusha sentensi hii katika nafsi ya kwanza, wingi. (alama 2)

Mlikinunua ili mtoto alalie.

(g) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 3)

ala ngombe aliyenunuliwa tanzania siku ya ijumaa ameibwa mchungaji alisikitika

(h) Ainisha maneno katika sentensi hii. (alama 4)

Salaale! Mtoto mdogo ameangushwa na kuumizwa vibaya sana na lile jingine.

(i) Nyambua vitenzi hivi katika kauli zifuatazo. (alama 4)

	tendeka	tendesha
tendewa	_____	_____
andika	_____	_____
lala	_____	_____
oa	_____	_____
la	_____	_____

(j)Andika sentensi hii katika hali ya udogo. (alama 2)

Mbwa ndogo amekatwa mkia

(k) Sentensi zifuatazo ni za aina gani? (alama 3)

(i)Juma analima ilhali Kamau anavua samaki

(ii)Paka wetu amekufa

(iii)Kitabu kilichopotea kimepatikana jaani

(l) Tunga sentensi kudhihirisha ngeli ya nomino hii. (alama 2)

Nyua

(m) Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu. (alama 3)

Mahali humu ndipo tutakakochezea soka juma lijalo.

(n) Kamilisha methali hii. (alama 1)

_____**si mkulima.**

5. ISIMU JAMII

(a) Eleza mambo **matano** ambayo hutawala mazungumzo. (alama 5)

(b)Jadili sifa **tano** za sajili ya sokoni. (alama 5)

MTIHANI 4

UFAHAMU (ALAMA 15)
Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuata

Madhara ya sigara

Chimbuko la kuonekana kwa madhara ya tumbaku ilikuwa mwaka 1598 A.D. Madhara yake yaligundulika wakati ambapo makala ya kwanza ya kiafya iliandikwa nchini Uingereza ikieleza madhara ya sigara. Baada ya hapo zilifuatia tafiti mbalimbali zilizoendelea kugundua na kuelezea madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za tumbaku kwa binadamu. Matokeo ya tafiti hizo yaliwezesha baadhi ya nchi kama vile Denmark, Uholanzi na Sweden kutunga sheria zinazozuia matumizi ya sigara. Katika sura ya pili, baadhi ya serikali zilikwazwa kiuchumi kwa kukosa pato la kodi zitokanazo na sigara na bidhaa zingine za tumbaku.

Mashirika na kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji na uuzaji wa sigara hutenga fungu kubwa la fedha kwa ajili ya kutangaza bidhaa hiyo hatari kwa afya ya mwanadamu. Kila mwaka, Shirika la Afya Ulimwenguni hutenga siku maalumu ya kuelimisha jamii kuhusu athari za kiafya na madhara yatokanayo na matumizi ya tumbaku. **Maadhimisho** hayo hufanyika kila Mei 30 ya mwaka na kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa "Mkinge mwanamke kuwa mteja au kutumiwa kama mhamasishaji wa bidhaa zingine za tumbaku'.

Takwimu za shirika hilo zinabainisha kuwa asilimia 90 ya wavutaji sigara wameanzia umri wa miaka 18. Pia zimebainisha kuwa, kwa kila sekunde ipitayo, wastani wa mtu mmoja anafariki kutokana na madhara ya tumbaku. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025, vifo vitaongezeka kwa asilimia 70. Utafiti umebainisha ifikapo mwaka 2030, watu milioni 10 watakuwa wamefariki kutokana na kuvuta sigara.

Uvutaji sigara unasababisha magonjwa mengi kama vile saratani ya mapafu, wendawazimu, **kupooza,** matatizo ya mfumo wa hewa, kutoboka utumbo, kunyonyoka nywele, kupungua kwa nguvu za kiume, maradhi ya ngozi na kadhalika. Madhara ya tumbaku hayajitokezi mara moja. Huchukua kipindi kirefu hata miaka 30, hali inayowafanya wengi kufumbia macho tahadhari iliyopo, wakiendelea kuteketezwa na uvutaji sigara. Anayevuta sigara huathirika mapafu kutokana na moshi na tindikali – aina ya kaboni iliyomo kwenye tumbaku inayomzuia kupumua na mapafu yake huanza kutunga usaha. Hali hiyo huchangia mtu kupata athari nyinginezo kama vile kichomi, kifua kikuu na saratani. Chembechembe ya nikotini iliyomo katika tumbaku ni hatari kwa mvutaji kwani humpotezea mtu hamu ya kula na anapata maumivu makali ya tumbo.

Wakati wote, mvutaji sigara hutoa harufu mbaya mdomoni, hali ambayo haipendezi katika maisha ya mwanadamu, na pia, huwa anawadhuru wengine. Mtu huyo anapopumua huchafua mazingira kwa kupumua hewa chafu na mbaya zaidi ambayo huwadhuru watu walio karibu naye kama vile mwenza katika ndoa (mke au mume), watoto au marafiki.

Inaelezwa kuwa sigara huathiri akili ya mwanadamu kutokana na kuwepo kwa chembechembe za ulevi. Hali hiyo ipo zaidi mtu anapotumia sigara kwa mara ya kwanza kabisa. Utafiti wa kitaalamu umethibitisha watoto wanaolelewa katika mazingira ya wazazi wanaotumia sigara kuathirika mishipa inayosafirisha damu kwenda katika moyo. Hali hiyo husababisha kuharibika kwa mfumo wa usafirishaji damu mwilini kwa watoto hao na mwishowe wanakuwa wahanga wa maradhi tofautitofauti.

Katika sura ya pili ya kisaikolojia, watoto wanaokaa na wazazi wanaovuta sigara huishia kuifuata tabia hiyo na huo ndio huwa mwanzo wa kudhoofika kwa maadili. Kwa wajawazito, sigara ina madhara kama vile kuathiri ukuaji wa mimba na kondo la nyuma au *placenta* kwa Kiingereza na kushindwa kusafirisha chakula vizuri kutoka kwa mama kwenda kwa moto. Madhara mengine ni moto kuzaliwa na uzito pungufu, hivyo kuathiri ukuaji wake. Kwa hivyo, ni vyema kufahamu kuwa ingawa sigara ni bidhaa inayotumiwa kama uraibu wakati wa kuivuta, madhara yake ni janga kubwa linalopaswa kupigwa vita bila kuchoka.

Maswali

(a) Madhara ya sigara yalionekana mwaka gani ? (alama 1

(b) Ni nchi gani zilizokuwa za kwanza kubuni sheria mpya kuhusu uvutaji wa sigara ? (alama 1)

(c) Uvutaji wa sigara una athari gani kwa anayevuta ? (alama 5)

(d) Watoto wanaathiriwa vipi na sigara ? (alama 4)

(e) Thibitisha kwamba uvutaji sigara hugharimu pesa nyingi. (alama 2)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatayo kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

(i) Kupooza

(ii) Maadhimisho

LUGHA - SEHEMU B

(a) Kwa kuzingatia jinsi ya kutamka sauti za kswahili ni nini tofauti kati ya (alama 2)

(i) Irabu

(ii) Konsonanti

(b) Eleza maana ya dhana hizi (alama 2)

(i) Kiimbo

(ii) Shadda

(c) Taja vipashio vine vya lugha (alama 4)

(d) Andika sentensi zifuatazo katika hali timilifu (alama 2)

(a) Mabati yananunuliwa

(b) Baba atakwenda dukani

(e) Kanusha sentensi zifuatazo (alama 3)

(i) Nchi za Afrika mashariki zalemewa na madeni.

(ii) Mbu amemuuma mtoto.

(iii) Baba ameandika barua ndefu.

(f) Zigeuze sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopita (alama 2)

(i) Unapendelea kula nyama siku hizi.

(ii) Opiyo alipenda kujiingiza katikati kama mchuzi wa ugali.

(g) Andika kwa wingi (alama 2)

(i)Maziwa ya mtoto yalimwagwa na paka yule.

(ii)Uvivu wa Juma unakera.

(h) Akifisha sentensi zifuatazo (alama 2)

(i)nenda sokoni ukaninunulie sukari maziwa na mkate

(ii)Maadam umeshafika tuanze mkutano

(i) Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kuandika viambishi mwafaka kulingana na kitenzi (alama 5)

Kitenzi	Nafsi	Wakati	Kirejeshi	Kitendwa	Mzizi	kiishio
Aliyelima						
Aliyempiga						
Anaoupanda						
Alipika						
Nitavileta						

(j) Taja vipera vya fasihi simulizi (alama 2)

(k) Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo (alama 2)

Mama amepika chai tamu sana

Nitakutembelea kesho jioni

(l) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa (alama 4)

Piga -

Jenga –

Fagia –

Chora -

(m) Taja na ueleze dhima ya lugha (alama 2)

(n) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea (alama 2)

(i) Mchoraji yule anachora picha nzuri
(ii) Mpishi atapika chakula kitamu

(o) Bainisha maneno katika sentensi zifuatazo. (alama 4)

Salaala ! Majangili wamewaua ndovu kumi leo asubuhi
Wale watafungwa

FASIHI (ALAMA 15)

Taja majukumu matano ya fasihi ya kiswahili (alama 5)
Taja tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi (alama 10)

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Nunua sabuni mpya ya GRESHA. *It is new !* Harufu yake ni *poa*, inadumu siku yote, inalainisha ngozi. Ng'arisha nguo zako na sabuni ya GRESHA. GRESHA sabuni *poa !* Bei yake ni nafuu; shilingi 20/= tu. Kila mtu ainunua.

Maswali

(a) Hii ni lugha gani ? (alama 2)
(b) Eleza sifa za lugha hii. (alama 8)

Insha (Aalama 20)

Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya ……. "Nilipopokea mezani chakula kitamu nilikumbuka maisha magumu niliyoyapitia, nikatambua kuwa si rahisi kupata chakula kama hicho bila juhudi maishani."

MTIHANI 5

(I) INSHA (ALAMA 20)

Insha yako isipungue maneno 350.

Andika insha inayoafiki methali "Fadhila za punda ni mateke".

MATUMIZI YA LUGHA

a) Taja aina mbili kuu za sauti. katika kiswahili (ala.2)

b) Taja:

i) Irabu za mbele. (ala.2)

ii) Irabu ya kati (ala.1)

iii) Irabu za nyuma (ala,1)

c) Kiungo ambacho hutetemaka na kutoa sauti huitwaje. (ala.1)

d) Viungo ambavyo hutumika katika utamkaji wa sauti huitwa je? (ala1)

e) Taja aina mbili za konsonanti. (ala.2)

f) Andika konsonanti tatu mabazo ni vipasuo. (ala.3)

g) Toa mifano miwili ya sauti za nazali/ving'ong'o. (ala.2)

h) Suati mwambatano nini? (ala.1)

i) Taja vipashio vine vya lugha. (ala.4)

j) Tenganisha neneo lifuatalo katika viambiu vyake mbalimbali. (ala.3)

k) Eleza maana ya:

a) Kiimbo (ala1)

b) Shada (ala.1)

L) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. (ala4)

i) Ukuta mbao ulianguka ni huu

ii) Mwanagenzi Yule amepita mtihani vizuri

M) Sentensi zifuatazo ziko katika nyakati / hali gani? (ala.2)

a) Otieno hula samaki kila siku

b) Yeye anaandika t kitabu

n) Tambulisha manene mbalimbali katika sentensi zifuatazo. (ala.4)

i) Mwanafunzi mvumilivu alisoma vizuri.

ii) Yule ameongea manene mengi

o) Taja

p) Kanusha sentensi ifuatayo. (ala2)

i) Nyumba hiyo ifafunfuliwa

q) Eleza matumizi ya 'Koloni'

Kisha utungie sentensi. (ala.1)

FASHI SIMULIZI (ala. 15)

1. Fasihi simulizi ni nini? (ala.2)

2. Taja na ueleze majukumu matano ya fasihi simulizi (ala 8)

3. Eleza tofauti tano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi (ala10]

4. Taja tanza nne kuu za fasihi simulizi. (ala.4)

MTIHANI 6

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

a) Taja irabu ya kati. (Alama.1)

b) Toa mifano miwili miwili konsontanti zifuatazo: (Alama 4)

i) Vikwamizo

ii) Nazali

C) Kiimbo nini? (Alama 1)

d) Weka shadda panapofaa. (Alama.2)

i) Mkuu

ii) Kupatana

e) Taja vipashio vitatu vya lugha. (Alama 3)

f) Tambulisha aina mbalimbali za maneno katika sentensi ifuatayo. (Alama 5)
Mtoto Yule ameingia ndani ya shimo.
e) Badilisha sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya wingi. (Alama 4)

i) Paipai hili lilinululiwa jana.

ii) Unyasi mrefu utakatwa kwa upanga.

f) Silabi ni nini? (Alama 2)

g) Andika neno lenye muundo wa : (Alama 2)

i) I + I

ii) K+ I+K+K+I

h) Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)

Wote wawili walimwona huyo.

i) Kanusha sentensi zifuatazo. (Alama 4)

a) Yeye anaimba vizuri.

b) Nyumba kubwa itajengwa

j) Tunga sentensi moja moja kutofautisha maneno yafuatayo. (Alama 2)

a) Vua

b) Fua

k) Eleza maana ya semi zifuatazo: (Alama 2)

i) Enda mrama

ii) Pata afueni

l) Onyesha kielezi (E) katika sentensi ifuatayo: (Alama 1)

Nyanya alitembea polepole.

m) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya alama ya nukta pacha.

n) Yakinisha sentensi ifuatayo. (Alama 2)

Maandishi yake hayaja pendeza mwalimu

o) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli uliyopewa mambanoni (1)

i) Futa(tendeka) ½

ii) Chagua (tendea) ½

FASIHI SIMULIZI

a) Eleza majukumu matatu ya fasihi simulizi. (Alama 3)

b) Taja vipera vinne vya fasihi simulizi. (Alama 4)

c)i) Hekaya ni nini? (Alama 1)

ii) Eleza umuhimu wa hekaya. (Alama 3)

d) a) Hurafa ni nini? (Alama 1

b) Eleza sifa tatu za hurufa. (Alama 3)

ISIMUJAMII

a) Ni nini maana ya Isimu jamii? (alama 2)

b) Taja kaida nne za lugha (alama 4)

c) Eleza sifa nne za sajili ya hospitalini. (alama 4)

MTIHANI 7

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Nairobi, mji mkuu wa Kenya ,ni jiji la maajabu na mastaajabu chungu nzima.Nadhari ya mtu anayewahi kuingia jiji hili kwa mara ya kwanza huvutiwa na huo msheheneko wa majumba ya fahari, marefu ajabu ,kiasi chaminazi mitano-sita ,iliyounganishwa kuelekea juu. mbinguni.

Jumba linalowavutia watu wengi ni lile la makongamano ya kimataifa liitwalo kwa Kiingereza Kenyatta International Conference Centre Jumba hili,hadi miaka michache iliyopita, ndilo lililokuwa refu zaidi mjini Jumba lenyewe- lina ghorofa ishirini na tisa hivi ,usipohesabu hilo pambo kama kofia kileleni mwake,linalojulikana kama mwavuli. Hata hivyo ,miaka michache iliyopita jengo hili lilipitwa urefu na Mnara wa Nyakati (Times Tower).Mnara huo hasa ni jumba linaloafiki lakabu yake ya kikwaruza mawingu.Jumba hili lina ghorofa zisizopungua thelathini na mbili.

Mbali na majumba haya mawili ,kuna majumba mengine zaidi ya ishirini katikati ya jiji ambayo ,japo mengine ni mafupi kiasi ,yana maumbo ya kustaajabisha kweli kweli.Hebu zingatia mwenyewe jumba liitwalo "mdomo wa kengele" au "bell —bottom" ambalo ni vioo vitupu ,toka chini hadi juu.Fauka ya ,umbo lake ni la kipekee ulimwenguni kote. Jumba hili lina kama miguu, kisha kiuno mithili ya kinu hivi japo si mviringo.Linapaa juu ,mbali sana ,likichukua umbo pana kuliko lilivyo chini;umbo la fua pana kama kengele.

Halafu rudia barabara .hizi hazina hesabu katikati ya jiji na ni pana, tena safi sana.Magari yanayotumia barabara hizi ni kochokocho,ya kila ama yanashindania nafasi,

Ajabu kubwa ya Nairobi hata hivyo ni idadi ya watu.Hakuna hasa anayejua idadi kamili ya watu wa Nairobi ,lakini sio kupiga chuku ninaposema kwamba ,hasa nyakati za kuelekea kazini asubuhi ,kwenda kula chakula cha mchana ,kuelekea nyumbani baada ya kazi na kuvuka barabara wakati wa msongamano, watu hukanyangana .Mtu anayesema kwamba watu wa Nairobi ni wengi kama chungu ,au kama mchanga wa ufuo wa bahari, hatii chumvi.

Watu wa Nairobi ,kwa tabia na mavazi, si kama watu wa kwingineko nchini Kenya .Watu hawa huvalia nadhifu sana.Wanawake ni warembo ajabu na hutengeneza nywele zao mithili ya hurulaini peponi.Wengi huvaa suruali ndefu. Kucha zao na midomo yao hupaka rangi maridadi sana.Huzungumza Kiswahili na Kiingereza takriban wakati wote.Wanawake wengi ajabu huendesha magari yao wenyewe ,jambo ambalo litakushangaza mara tu uingiapo jijini ,hasa kama ulilelewa ukidhani maskani mwafaka ya wanawake ni jikoni peke yake;yaani kuzingatia ile falsafa kuwa "kuoa ni kupata jiko".Wanaume nao huvaa suti safi ,maridadi na shingoni wamefunga tai stahiki yao.Wanaume hao huendesha magari na kuyaegesha karibu na afisi zao.Huingia afisini mwao kwa maringo na madaha,huku funguo za magari yao zikining'inia vidoleni. Hawa nao husema na Kiingereza kupitia puani, utadhani ni waingereza hasa.

Kwa upande mwingine ,watoto ni nadhifu kweli kweli hasa watoto wa shule.Hawa huvalia sare zilizofuliwa na kunyoshwa vizuri kwa pasi. Wake kwa waume ,shingoni huvalia tai Watoto wa shule za Nairobi huongea Kiswahili, Kiingereza na sheng,ambayo ni "lahja" yao waliyoibuni."Lahja" hii ni mchanganyiko wa Kiswahili,Kingereza na msamiati

mchache wa lugha nyingine za Wakenya zisemwazo jijini Nairobi na vitongoji vyake.

Kwa jumla ,watu wote wa Nairobi hutembea kasi sana.Hawana hata wakati wa kutembea polepole na kuangazaangaza huku na huko.Iwapo wewe ni mgeni jijini,ukizubaa utapigwa kumbo na waendelee na hamsini zao kama vile hapakutokea jambo.Hili linapojiri, usidhani limefanywa maksudi.La, hasha.Ni vile tu kwamba Wanairobi hawana muda wa kupoteza.

Maswali

(a) Kwa nini majumba ya jiji la Nairobi yana majina au lakabu za Kiingereza? (ala 2)

(b) (i) Baadhi ya maajabu ya Nairobi ni barabara safi, msongamano wa magari na majumba marefu. Ongezea maajabu mengine matatu. (ala 3)

(ii) Watu wa Nairobi wanajipenda kweli kweli, Fafanua (ala 3)

(c) (i) Je, Unadhani watu wa Nairobi kweli hukanyagana? Eleza ni kwa nini msimulizi ametoa maelezo hayo (ala 1)

(ii) Unafikiri ni kwa nini hasa wanawake wa Nairobi wanaonekana nadhifu? (ala 2)

(d) Kwa nini neno "lahja" limewekwa alama za mtajo? (ala 1)

(e) Eleza maana ya maneno na tamathali za usemi zifuatazo. (ala 3)

(i) Nadhari

(ii) Linaloafiki

(iii) Waendelee na hamsini zao

2. UFUPISHO

Kiswahili nchini Kenya kilisambazwa kwa njia ya biashara kutoka upwa wa Kenya kwenda bara yake ,ingawa si kwa wingi sana kwa sababu wenyeji wa upwa wa Kenya —Mombasa, Siu na Pate-walikuwa katika vita vya kupigana na utawala wa Kisultani wa Seyyid Said, Sayyid Majid na Seyyid Barrgash.Hata hivyo kuna baadhi ya misafara iliyokwenda bara na kueneza Kiswahili.Kwa mfano, Waswahili wa kutoka Jomvu na Mvita walifanya biashara na Wakamba.Baadhi yao walioa Ukambani na mpaka wa leo kuna milango ya Waswahili ambao nyanya zao wanatoka Ukambani.Wafanyabiashara wengine Waswahili walifika mpaka Umaasaini.

Utawala wa kikoloni ulikitweza sana Kiswahili. Waingereza walitilia mkazo utumiaji wa lugha za kikabila kwa vile walisema kwamba mtu angeeleza hisia zake vizuri kwa kutumia lugha yake ya kwanza.Kiswahili kilitwezwa na kuchukuliwa kuwa ni lugha ya maboi.Wajerumani walikitweza sana nchini Kenya.Wamisheni pia walikipinga Kiswahili kwa sababu ya ufungamanao na Uislamu,

Hata hivyo, Kiswahili kilikuwa kinatumika katika mawasiliano, kwa hivyo wakakata shauri kwamba kitumike katika kufundashia shuleni.Lugha za makabila zilitumiwa katika madarasa ya chini-Kiswahili katika madarasa ya kati, na Kiingereza katika madarasa ya juu.Mtihani wa Kenya African Preliminary Examination (KAPE), ulikuwa ukifanywa katika lugha ya Kswahili nchini Kenya, uliondolewa,

Kiswahili kilitumika katika kuwaunganisha wakenya katika shughuli za ukombozi wa nchi na pia kama lugha ya umma.Mnamo mwaka wa 1964,Tume ya Ominde ilipendekeza kwamba Kiswahili kitumike kwa vile ndiyo lugha ya kumuunganisha Mwafrika, na pia ingetuwezesha kuwasiliana na nchi zingine za Afrika Mashariki na Kongo,

Mnamo mwaka wa 1969, chama cha Kenya National Africa Union (KANU) ,kilifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa, Raisi wa kwanza wa KANU alikuwa akitolea hotuba zake nyingi katika lugha ya Kiswahili, na alitoa kwa Kiingereza kwa ajili ya mabalozi tu.Fasihi ya Kiswahili ilianzishwa mwaka wa 1973, na kwa hivyo wanafunzi wakaanza kuifanya katika kidato cha nne na cha sita.

Ingawa Kiswahili kilitwezwa sana na Waingereza, bado kinatumika na watu wengi kama lugha ya mawasiliano.Mwaka wa 1968, Berndt Heine alifanya uchunguzi na aliona kwamba asilimia 85.25 ya Wakenya hutumia Kiswahili kama lugha yao ya pili na ndiyo lugha ya mawasiliano.Hivi sasa lugha ya Kiswahili imepewa kipaumbele;ni

lugha ya taifa na pia lugha rasmi.Katika sekta ya elimu,Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msimgi na za sekondari.Ni somo ambalo linanaendeelezwa hata katika vyuo vikuu vya Kenya.

Ni muhimu kutaja kuwa Kiswahili hakikuenea katika bara ya Kenya kama kilivyoenea Tanganyika. Kiswahili kilienea sana Tanzania kwa sababu ya wakoloni, yaani Wajerumani,waliosisitiza matumizi ya Kiswahili;lakini Waingereza walikitweza katika nchi ya Kenya

Licha ya hayo,nchi ya Tanzania ina lugha 120, na Kenya ina lugha kama 41.Nchi ikiwa na lugha nyingi na watu wachache wanaoitumia kila mojawapo ya lugha hizi,ni rahisi kukuza au kuinua lugha moja kuwa lugha ya taifa inayotumiwa na watu wengi.Hoja hii ilifanya Kiswahili kisienee sana Uganda na Kenya ,lakini kikaenea sana Tanzania.

Kiswahili hakikuenea sana nchi ya Kenya kwa sababu biashara haikufana sana katika pwani ya Kenya kama mji wa Unguja.Wanyamwezi na Wayao waliokuwa wakishughulika na biashara huko Tanzania walieneza Kiswahili katika bara, jambo ambalo Wakamba walioshughulika na biashara Kenya hawakushughulika nalo.Wakamba hawakuiga lugha ya watu wa pwani,Wamaasai waliogopwa sana na wafanyabiashara,na kwa hivyo biashara haikufana sana.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa fupisha aya ya kwanza na ya pili (maneno 50-60) 7

(b) Kwa kuzingatia aya za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi (maneno 60 – 70) (ala 8)

MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) Eleza tofauti kati ya sauti /z/ na /d/ (ala 1)
(ii) Toa kigezo chochote kimoja cha kuainishia konsonanti. (ala 1)

(b) Sentensi ifuatayo ina maana mbili tofauti. Zieleze. (ala 2)
Huyu amekuja kutuliza.

(c) Ikanushe sentensi ifuatayo kwa udogo. (ala 2)
Nyumba yenyewe ilijengwa bondeni karibu na mto.

(d) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo: (ala 2)
(i) Mbono (mti)
(ii) Barabara (sawasawa)

(e) Andika sentensi kuonyesha matumizi mawili ya:
(i) Kinyota (ala 2)
(ii) Ritifaa . (ala 2)

(f) Tunga sentensi mbili tofauti zinazobainisha maana tofauti kati ya (ala 2)
(i) Nduni
(ii) Duni

(g) Taja aina zozote mbili za sentensi. (ala 2)

(h) Andika sentensi ifuatayo iwe katika hai ya -ki- ya masharti (ala 2)
Tulilala sana tukachelewa kwenda shuleni.

(i) (1) Taja aina nne za nomino. (al2)
(2)Tambua aina za vihusishi vilivyo pigwa mistari katika sentensi zifuatazo. (al2)
(a)Hassan anacheza vizuri **kuliko** Kiprini.
(b)Simtambui **kwa vile** amebadilisha nguo.

(j) Taja ngeli za nomino zifuatazo (ala 3)
(1)Ujinga (2)Ugonjwa (3)Kucheza (4)Sukari (5)Barua (6)Mti

(k) Tunga sentensi ukitumia nomino ifuatayo pamoja na kivumishi kisisitizi cha mbali kidogo, Mgomba (ala 2)

(l) Tunga sentensi mbili ukitumia neno kisabuni kama: (ala 2)
(i) Nomino
(ii) kielezi

(m) Andika visawe vya (ala 2)
(i) Hidaya
(ii) Ngeu

(n) Iandike sentensi ifuatayo upya ukitumia ‘0” rejeshi tamati (ala 2)
Chumvi iliyochafuka si ile unayoizungumzia.

(o) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo (ala 2)
Mwanasiasa shupavu aliyewachochea wananchi amekamatwa.

(p) Yakinisha sentensi ifuatayo katika umoja (ala 2)
Nyuzi zisingekatika zisingepotea.

(q) Taja matumizi ya kiambishi ku_ (ala 1)

(r) Taja aina mbili za mofimu (ala 2)

4. **ISIMU JAMII**

a. Taja sababu mbili zinazomfanya mzungumzaji kutumia zaidi ya lugha moja katika mazungumzo (ala 2)

b. Kwa kutoa mfano, eleza maana ya uwingi lugha. (ala 2)

c. Fafanua mambo sita yanaoweza kuifanya lugha yeyote ife, (ala 6)

MTIHANI 8

MASWALI YA FASIHI SIMULIZI

1. **Swale la 1**
   a) Fafanua sifa tatu za kila mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi vifuatavyo (alama6)
      (i) Vitendawili
      (ii) Methali
   b) Mawaidha yana dhima gani katika jamii? Eleza (alama6)
   c) Bainisha sifa za nyimbo. (alama4)
   d) Eleza umuhimu wa nyimbo za kisiasa (alama4)

2. **Swali 2**
   a) Eleza namna ambavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji. (alama 8)
   b) Taja sifa nne bainifu za hadithi. (alama 4)
   c) Fafanua sifa nne za fanani/mtambaji bora. (alama 8)

3. **swali 3**
   a) Methali ni nini? (alama2)
   b) Ainisha sifa Tano za methali za Kiswahili (alama10)
   c) Elezea umuhimu wa hadithi kama utanzu wa fasihi simulizi katika jamii (alama8)

4. **Swali la 4**
   a) Maghani ni nini? (alama 2)
   b) Eleza fani zifuatazo za maghani (alama 8)
      1. Vivugo
      2. Tondozi
      3. Pembezi
      4. Rara
   c) Eleza maana ya neno ULUMBI (alama 1)
   d) Bainisha sifa za mlumbi (alama 6)
   e) Eleza umuhimu wa ulumbi (alama 3)

5. **Swali la 5**
   a) **Taja** mbinu zozote tatu za kuhifadhi fasihi simulizi (alama 3)
   b) Taja aina zozote tatu za vitendawili (alama 3)
   c) Bainisha matumizi ya lugha katika vitendawili (alama 3)
   d) Ngomezi ni nini? (alama 1)
   e) Eleza ujumbe uliowasilishwa na ngomezi katika fasihi simulizi. (alama 3)
   f) Fafanua sifa zozote nne za ngomezi. (alama 4)
   g) Taja mifano mitatu ya ngomezi ya kisasa. (alama 3)

6. **Swali la 6**
   a) Tofautisha baina ya
      (i) Hurafa na Hekaya. (alama 4)
      (ii) Hadithi za mazimwi na hadithi za mtanziko. (alama 4)
      (iii) Usuli na visasili. (alama 4)
   b) He! He! He! Weee!
      Unayeogopa kutahiriwa
      Nani atatahiri badala yako
      Eh, eh.... Ni babu yako

Eh, Eee!.... kisu kikali mno!
Lakini nitavumilia.
(i) Wimbo huu huitwaje? (alama 1)
(ii) Nini dhamira ya wimbo huu? (alama 2)
(iii) Taja sifa zozote tano za utanzu wa nyimbo kwa jumla.(alama 5)

7. Swali la 7

a) (i) **Eleza** maana ya misimu (alama 1)
(ii) Kuchipuka kwa misimu kunategemea mambo mengi. **Taja** matano miongoni mwa haya. (alama 5)
b) **Eleza** muhimu wa misimu katika jamii (alama 4)
c) (i)Nini maana ya ngomezi? (alama 2)
(ii) Ngomezi ina umuhimu gani? (alama 5)
d) **Taja** udhaifu wa ngomezi katika kuwasilisha ujumbe katika jamii (alama 3

8. Swali la 8

a) (i) **Fafanua** maana ya methali (alama 2)
(ii) **Fafanua** sifa tano za methali (alama 5)
b) **Eleza** majukumu matano ya methali
c) **Eleza** jinsi fasihi simulizi inavyohifadhiwa siku hizi
d) **Taja njia nne** za kukusanya fasihi simulizi

9. Swali 9

a) Taja majukumu manne ya Fasihi Simulizi. (alama 4)
b) (i) Mawaidha ni nini? (alama 1)
(ii) Fafanua sifa tatu za mawaidha. (alama 3)
c) Eleza maana na umuhimu wa aina hizi za nyimbo.
(i) Nyiso (alama 2)
(ii) Mbolezi (alama 2)
(iii) Vave (wawe) (alama 2)
d) Taja vijipera vitatu vya maigizo. (alama 3)
e) Fafanua sifa tatu za methali. (alama 3)

10. Swali la 10

a) Tofautisha baina ya ulumbi na soga (Alama 4)
b) Fafanua sifa za ulumbi (Alama 7)
c) Taja baadhi ya Miviga maarufu katika jamii za Afrika (Alama 3)
d) Eleza umuhimu wa Miviga katika jamii (Alama 6)

11. Swali la 11

a) Eleza maana ya tanzu zifuatazo za Fasihi Simulizi(alama 4)
i. Vitanza ndimi
ii. Vitendawili
iii. Ngano
iv. Nyimbo
b) Taja sifa mbili mbili za kila mojawapo wa vipera vya fasihi simulizi vilivyotajwa kati (alama 8)
c) Eleza umuhimu wa vitanza ndimi. (alama 4)
d) Fafanua uamilifu wa vitendawili katika jamii. (alama 4

12. Swali la 12

a) Maghani ni nini? (alama 2)
b) Eleza fani zifuatazo za maghani
i. Vivugo
ii. Tondozi
iii. Pembezi
iv. Rara (alama 8)
c) Eleza maana ya neno **ULUMBI** (alama 2)
d) Bainisha sifa nane za mlumbi (alama 8)

13. SWALI 13

a) Fasihi simulizi ina makundi manne makuu, yataje. alama 4
b) Kwa kila kikundi ulichotaja katika swali la (a) , toa mifano miwili ya vipera vya kila kikundi na utoe maelezo mafupi ya vipera hivyo alama 8
c) Nyimbo huwa na jukumu gani katika usimulizi alama 2
d) Fasihi simulizi ina sifa ya kuhifadhiwa akilini . Eleza udhaifu wa uhifadhi wa akilini. Alama 6

14. SWALI 14

a)Taja mbinu zozote nne zinazotumiwa kuhifadhi fasihi simulizi huku ukitolea mifano

(alama 4)

b) Eleza umuhimu wa kuhifadhi fasihi simulizi (alama 8)

c)Semi ni utanzu wa fasihi simulizi ambao ni mfupi na uundwao kwa maneno machache au sentensi kadha.Taja na ujadili vipengele vyovyote vinne vinavyojumuishwa na kundi hili(alama 8)

15. SWALI 15

a) Tofautisha kati ya methali na msemo. (alama 2)

b) Toa mifano miwili miwili ya methali zinazozingatia tamathali zifuatazo;

i. Balagha (alama 2)

ii. Takriri (alama 2)

iii. Ukinzano (alama 2)

c) (i) Fafanua vijipera vifuatavyo vya mazungumzo.

i. Utani (alama 2)

ii. Soga (alama 2

iii. Ulumbi (alama 2)

iv. Taja sifa na umuhimu wa soga. (alama 6)

16. SWALI 16

a) Eleza kikamilifu sifa zozote tano za mtambaji katika fasihi simulizi(alama 10)

b) Fasihi simulizi aghalabu hutambulika kutokana na sifa zake kuu. Jadili.(alama10)

17. Swali la 17

a) Ngomezi ni nini? (alama 2)

b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamii. (alama 4)

c) Methali zina umuhimu gani katika jamii? (alama 10)

d) d) Eleza jukumu la fomula za ufunguzi katika hadithi.(alama 4)

18. SWALI 18

a. **Taja** mifano minane ya tanzu fupi katika fasihi simulizi.

b. **Fafanua** sifa zozote tatu za mawaidha katika fasihi simulizi.

c. **Eleza** umuhimu tatu wa ngomezi. (alama 3)

d. **Eleza** istilahi hizi za fasihi simulizi. (alama 3)

i. Maghani

ii. Mapisi

iii. Misimu / simo

e. **Fafanua** sifa zozote tatu ambazo mtambaji wa hadithi anastahili kuwa nazo. (alama 3)

f. **Taja** methali zozote mbili zilizo na dhana ya tashibiha. (alama 2)

g. **Eleza** sifa zozote mbili za nyimbo zinazotofautisha nyimbo na ushairi simulizi (alama 2)

19. SWALI 19

a) Taja na ueleze aina zozote tano za Hadithi. (alama 5)

b) Tofautisha kati ya

i. Mbolezi na Bembezi

ii. Vitendawili na chemsha bongo. (alama 4)

c) Eleza umuhimu wa vitanza ndimi (alama 3)

d) Taja na ueleze sifa nne ambazo mtambaji anapaswa kuwa nazo.(alama 4)

e) (i) Fafanua maana ya methali. (alama 2)

(ii)Taja methali zinazohusu: ***Kuliwaza.***

20. SWALI 20

a) (i)Ngano ni **nini**? [alama 1]

(ii)Eleza tofauti iliyoko kati ya visasili na visakale [alama 4]

(iii)Fafanua majukumu yoyote muhimu ya ngano katika jamii. [alama 5]

b) (i) **Eleza** umuhimu wa vitendawili katika jamii. [Alama 3]

(ii) **Tega** na **utegue** vitendawili vyovyote viwili vilivyo na lugha ya takriri na lugha ya mlio.[alama 2]

c) **Taja** sifa zozote tatu za methali. [alama 3]

d) **Taja** methali yoyote iliyo na lugha ya balagha kisha ueleze maana yake ya ndani [alama 2]

21. Swali la 21

a) (i) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi.(Alama 2)

(ii) Taja na kueleza tanzu / aina za nyimbo (Alama 10)

b) Tofautisha semi hizi

i) Nahau na misimu (Alama 2)

ii) Eleza maana ya nahau hizi (Alama 4)

a. Hawapikiki katika chungu kimoja

b. Yeye ni jamvi la wageni

c. Amemwaga mtama
d. Amechomekwa mizizi

c) Taja na kufafanua misimu yoyote miwili. (alama 2)

22. SWALI 22

a) Fafanua fani zifuatazo za fasihi simulizi (alama 6)
   i. Ngano za mtanziko
   ii. Mazingira
   iii. Kifunga nyama

b) Umeombwa kusimulia darasani mighani wa Fumo Liyongo, eleza namna utakavyofanikisha uwasilishaji wako. (alama10)

c) Je, ni vipi jamii ya kisasa inaendeleza Fasihi Simulizi (alama 4)

23. SWALI LA 23

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu

Ulojipambanua kwa mabingwa

Wachezaji hodari wa ngoma

Ndimi dume liloingia nyanjani

Makoo yakatetemeka

Yakang'ang'ania gozi kusakata nami

a. Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki. (alama 2)
b. Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi.(alama 10)
c. Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 8)

24. SWALI LA 24

a) Taja na ueleze vipera vya maghani. (alama 10)

b) Eleza maana ya miviga. (alama 2)

c) Fafanua sifa nne za miviga katika jamii. (alama 8)

25. SWALI LA 25

a) Huku ukitoa hoja sita linganisha aina mbili kuu za fasihi.(alama 6)

b) Jadili vipengele sita vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi.(alama 6)

c) Jadili sifa mbili za vitanza ndimi kwa kurejelea sauti.(alama 2)

d) Tambua istuiatu zinzotokana na maelezo haya.

(i) Msimulizi wa fasihi simulizi anaitwaje kwa jumla? (alama 1)

(ii) Shujaa katika mighani pia anaweza kuitwa nani?(alama 1)

(iii) Sherehe za kitamaduni ambazo hufungwa na jamii katika kipindi fulani maalum huitwaje? (alama 1)

(iv) Mavazi au vifaa vinavyotumiwa na wasanii kuakisi hali halisi ya mambo wakati wa kuwasilisha fasihi huitwaje? (alama 1)

(v) Mtambaji wa hadithi hutumia ujuzi gani anapoibadilisha hadithi yake moja kwa moja mbele ya hadhira bila kuathiri usimulizi wake?(alama 1)

(vi) Wanaosimuliwa ili kuonyesha kazi ya fasihi simulizi hupewa jina hili. (alama 1)

26. SWALI LA 26

a) Eleza sifa tano za miviga. (alama 5)

b) Huku ukitoa mifano, onyesha udhaifu wa miviga. (alama 5)

c) Taja aina za miviga ambayo hupatikana katika jamii ya kisasa. (alama 5)

d) Eleza nafasi ya miviga katika jamii. (alama 5)

27. SWALI LA 27

a) Eleza vipengele vitano vya fasihi simulizi ambavyo hujitokeza katika fasihi andishi. (alama 10)

b) Fafanua sifa tano za ushairi simulizi.(alama 10)

28. SWALI LA 28

a) Fafanua mambo yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (alama 10)
b) Eleza maana ya lakabu. (alama 2)
c) Sifa za lakabu ni zipi? (alama 4)
d) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii. (alama 4)

29. SWALI LA 29

a) Eleza maana ya maigizo katika fasihi simulizi.(alama 2)

b) Tofautisha aina mbili kuu za maigizo. (alama 8)

c) Kwa kutoa hoja sita, eleza umuhimu wa maigizo katika jamii.(alama 6)

d) Kwa kutoa mifano minne, onyesha jinsi misimu huzuka.(alama 4)

30. SWALI LA 30

a) Miviga inafaaa kupigwa marufuku katika jamii ya kisasa. Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nane (alama 8)

b) Taja mifano sita yangomezi za kisasa (alama 6)

c) Ni jukumu la jamii kudumisha Fasihi Simulizi. Dhihirisha (alama 6)

31. SWALI LA 31

Ewe malaika wangu

Uloshuka toka mbinguni

Mbingu kapasua kwa heri

Siku nipokukopoa

Ulinitia furaha iliyopasua kifua

Tabasamu kipajini pako

Ilinitia tumaini, ikanisahaulisha zingizi

Ikayayeyusha madhila, ya utasa wa miaka kumi

Ikapeperusha mbali, cheko la ukewenza.

Sasa napolia, wanitonesha jeraha

Wanirejesha misri, kwa vitimbi vya Firauni

Kwa vitisho vya muhebi

Talaka kuahidiwa, hadi mbingu

Lipofungua milango ya heri.

Silie mwana silie, walimwengu watakusuta,

Tangu hapo tanabahi

Vidume humu mwenu

Kulia havikuumbiwa,

Machozi na kekevu ni za kike fahamu,

Jogoo halii daima huwika

Nikikuona kigugumika hivi wanitia hangaiko

Tumaini kuzima

Udhaifu kiandama

Moyo kutia hamaniko,

Ananipigania nani?

Watesi king'ang'ania

Changu kujitwalia?

Maswali.

a) Thibitisha aina ya utungo huu. (alama 2)

b) (i) Bainisha jinsia inayoongolewa kwenye utungo huu. (alama 1)

(ii) Thibitisha jibu lako la hapo juu (i) (alama 1)

c) (i) Elesa nafsineni katika utungo huu. (alama 1)

(ii) Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako la hapo juu (i) (alama 1)

d) Eleza sifa tano za utungo huu. (alama 5)

e) Huku ukitoa mifano, bainisha vipengele sita vya kimtindo ambapo nafsineni imetumian kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 6)

f) Eleza majukumu tano ya utungo huu. (alama 5)

32. SWALI LA 32

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Sungura alivyokwepa kuliwa na simba

Wanyama wa pori waliamua siku moja kumtuma mnyama mmoja kila siku alikoishi simba kama chakula. Siku moja ilikuwa zamu ya sungura kwenda huko. Sungura alikuwa mjanja sana. Alipanga mpango mzuri wa kumwangamiza simba.

Alienda alikoishi simba muda mrefu baada ya muda wa chakula wa simba. Alimkuta simba akiwa na hasira kubwa sana.

``Kwa nini umechelewa jinsi hii?`` aliuliza kwa hasira.

'Bwana wee,`` alisema sungura kwa sauti ya upole.

``Nilichelewa kwa sababu simba mwingine alinikimbiza. Nilitaabika sana kabla ya kupata upenyu wa kutoroka.``

``Simba mwingine? Je, katika pori hili?`` aliuliza samba.

``Ndiyo bwana mkubwa. Najua anakoishi. Tuandamane nikakuonyeshe,`` alisema sungura.

Simba alijitayarisha kuandamana na sungura. Sungura aliongoza njia hadi walipofika mahali palipokuwa na kisima kikubwa. Sungura alimgeukia na kusema, ``Anaishi hapa. Tafadhali njoo umuone!``

Simba alisogea ulipokuwa ukingo wa kile kisima. Aliyatupa macho huko na kukiona kivuli chake. Alidhani kuwa huyo alikuwa simba mwingine. Kwa hasira kubwa alifungua kinywa na kunguruma. Alimwona huyo simba mwingine akikenulia meno. Simba hakuweza kusubiri, alijitosa kisimani apambane na simba huyo. Huo ulikuwa mwisho wake.

Sungura aliondoka akicheka akifurahi kuwa sasa wanyama hawataliwa tena na simba.

Maswali

a) i) Andika aina ya hadithi hii (alama 1) ii) Taja sifa tatu za kutambulisha aina hii ya hadithi (alama 3)
iii) Fafanua umuhimu wa aina hii ya hadithi kwa jamii (alama 3)

b) Kwa kutoa mifano taja aina mbili ya fomyula ya: (alama 4)
i)Kuanza hadithi
ii) Kumalizia hadithi

c) Eleza sifa nne za mtambaji bora katika fasihi simulizi (alama 4)

d) Tofautisha kati ya vipera viwili vya fasihi simulizi.
i)Mighani na maghani (alama 2)
ii) Lakabu na misimu (alama 2)

33. SWALI LA 33

a) Taja aina nne za nyimbo (alama 4)

b) Eleza umuhimu wa nyimbo katika jamii (alama 8)

c) Taja na udhibitishe sifa nne za kimtindo za methali. (alama 8)

34. SWALI LA 34

(a) Fafanua maana ya Hodiya katika jamii nyingi za kiafrika. (alama.2)
(b) Fafanua sifa zozote nne za hodiya katika jamii husika, (alama.8)
(c) Hodiya ilikuwa na umuhimu upi katika jamii husika. (alama 10)

35. SWALI LA 35

(a) Maigizo ni nini ? (alma 2)
(b) Tofautisha aina mbili kuu za maigizo (alama 8)
(c) Eleza umuhimu wa michezo ya watoto katika jamii husika (alama 10)

36. SWALI LA 36

Soma hadithi hii kasha ujibu maswali

Ilikuwa alfajiri yenye baridi. Umande ulitapakaa kote. Ukungu ulitanda hivi kwamba hungeweza kumuona mtu alikuwa hatua chache mbele yako. Ndovu alipoamka, alikuta fisi mlangoni pake. Fisi alikuwa amemlimia ndovu shamba lake, lakini alikuwa hajalipwa ujira wake.

Kila alipomwendea ndovu kwa ajili ya malipo yake, fisi alitiliwa huku na kutolewa kule."Leo ni leo",fisi alimwambia ndovu."Nimevumilia vya kutosha. Kila siku ninapokuja kuchukua pesa zangu, hukosi hadithi mpya ya kunisimulia. Leo sitoki hapa bila pesa zangu!"

Fisi alipomaliza kumwaga joto lake, ndovu alimwambia: "Sikiliza fisi. Mimi nimeheshimika kote kijijini. Naona haja yako ni kunivunjia heshima –mbele ya familia yangu na wanakijiji kwa jumla. Sikulipi pesa zako, mpaka ujifunze kuwaheshimu wazee. Nakuamuru uondoke hapa mara moja, kabla sijakasirika! Nataka uende popote, unapofikiria kwamba unaweza kupata msaada. Ukienda kwa chifu, usisahau kwamba tunakunywa na yeye. Ukienda polisi, mkuu wa kituo amejaa tele mfukoni mwangu. Ukienda mahakamani, hakimu tulisoma darasa moja. Popote uendapo, hakuna yeyote atakayekusikiliza"

"Zaidi ya hayo, hakuna yeyote atakayekuamini.Mimi naitwa Bwana pesa.Kwangu umeota mpesapesa na kustawi. Nani ataamini kwamba naweza kushindwa kulipa vijisenti vichache ninavyodaiwa na fisi?"

Fisi alisikiliza kwa makini majitapo ya ndovu. Aliamua kumpasulia ndovu mbarika: "Bwana ndovu najua kuwa wewe una nguvu na uwezo mkubwa wa kifedha.Lakini hayo yote mimi hayanihusu ni yako na familia yako. Sitakuruhusu unidhulumu kilicho haki yangu. Usiutumie uwezo uliopewa na Muumba kuwaonea na kuwanyanyasa maskini wasio mbele wala nyuma" alimaliza usemi wake na kuondoka huku machozi yakimdondoka.

Fisi alipofika nyumbani, aliwasimulia fisi wanyonge wenzake yaliyomsiba.Fisi walikusanyika na kulizingira boma la ndovu huku wakisema: "Tunataka haki itekelezwe! Dhuluma lazima ikome! Unyanyasaji lazima ukome!" Ndovu aliposikia kelele langoni mwake, alipiga simu kwenye kituo cha polisi.

Mara, kikosi cha polisi wa kupambana na ghasi kiliwasili. Fisi walipigwa mijeledi na kuezekwa marungu. Waliojifanya mabingwa walipigwa risasi. Fisi waliosalia walikimbilia makwao, huku wakichechemea kwa maumivu. Mpaka wa leo fisi wangali wanatembea kwa kuchechemea.

(a) Usimulizi huu ni wa aina gani? Toa sababu. (alama 2)
(b) Eleza tamathali za usemi zilizotumika katika hadithi hii. (alama 4)
(c) Eleza sifa za ndovu katika hadith hii. (alama 5)
(d) Fafanua jinsi kisa hiki kinavyo dhihirisha methali: 'Mwenye nguvu mpishe(alama3)
(e) Je, hadithi zina umuhimu gani katika jamii? (alama 6)

37. SWALI LA 37

(a) Eleza dhima nne za hojaji katika utafiti wa fasihi simulizi. (alama4)
(b) Fafanua vizisingizi vyovyote vinane katika ukusanyaji wa fasihi simulizi. (alama16)

38. SWALI LA 38

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata

Nimekuita hapa kwa sababu moja
Unaelewa kile ulichofanya!
Nimekupa muda wa kutosha kujiasa na kutambua
Haja ya kuomba msamaha lakini umepuuza!
Kama kweli wewe ni mwanafunzi wangu!
Nimekufunza maarifa, maadili na hata haja ya kufanya bidii masomoni.
Mara kadha nimekusaidia kihali na kifedha
Nimekutafutia wafadhili wa masomo yako
Sasa umesahau hayo yote!
Umeanza kunivunjia heshima.
Unanyemelea vitu vyangu na kuiba,
Ninapokuuliza unagombana nami kama mtoto wa rika yako!
Kule nje walichafua jina langu ukisema ati mimi ni mchawi.
Miungu nawaone chozi langu,
Wasikie kilio changu.
Mizimu na waone uchungu wangu
Radhi Baraka wala fanaka yoyote wasikupe
Usiwahi kufurahia hata siku moja masomo yako.
Na iwapo utakuwa mwalimu, wanafunzi wako wakutendee mabaya Zaidi!

MASWALI

(a) Tambulisha kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 2)
(b) Eleza sifa zozote tano za kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 10)
(c) Mbali na muktadha uliorejelewa taja kwa kutolea mifano miktadha mingine minne ambamo kipera hiki huhusishwa (alama 4)
(d) Taja umuhimu wa kipera hiki katika jamii (alama 4)

39. SWALI LA 39

" Ukichukua mama chukua na mtoto"

(a) Tambilisha kipera cha fasihi simulizi (alama 2)
(b) Fafanua sifa zozote tano za kipera hiki (alama 10)
(c) Eleza mambo yoyote manne yanayozingatiwa wakati wa kuainisha misimu (alama 8)

40. SWALI LA 40

(a) Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa. (alama 2)
(b) Eleza sifa **nne** za maapizo. (alama 2)
(c) Eleza kikwazo **vitatu** vinavyokumba Fasihi simulizi. (alama 3)
(d) (i) Ni nini maana ya vivugo (alama 1)
(ii)Eleza sifa zinazotambulisha vivugo (alama 4)
(iii) Fafanua majukumu ya vivugo (alama 8)

Kwa majibu ya maswali haya piga simu ama utume ujumbe kwa

BWANA CHEPKWONY COSMAS 0724351706 upate usaidizi

MTIHANI 9

MASWALI YA ISIMUJAMII

1. "Haya basi. Beba mmoja! Beba mmoja! Dada njoo. Nafasi ni ya mmoja. Ni mbao tu. Bei ya chini kuliko keki.

Usiachwe, bei ni poa."

a. Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)

b. Fafanua sifa nane za sajili hiyo. (alama 8)

2.

a) Ukiwa mkaguzi mwalikwa katika mashindano ya Kiswahili, fafanua na kueleza mambo yanayochangia wanafunzi kufanya makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili. Alama 5

b) Eleza umuhimu wa Isimu Jamii. (alama 5)

3. a) Eleza matatizo matano yaliyokumba maenezi ya Kiswahili kabla ya uhuru nchini Kenya (alama. 5)

b)Fafanua sifa tano za lugha inayotumiwa darasani (alama 5)

4. (a) Eleza dhana ya uwingi lugha. (alama 2)

(b) Fafanua mambo manne yanayochangia uwingi lugha katika jamii. (alama 8)

5. a)Eleza sababu tano zilizochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya Uhuru. (al.5)

b)Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kuikuzalugha ya Kiswahili baada ya Uhuru nchini Kenya. (al. 5

6. a) Eleza istilahi zifuatazo za isimu jamii. (al.4)

(i) Lugha ya taifa.

(ii) Lugha sanifu.

(iii) Lugha rasmi.

(iv) Lahaja.

(b) Fafanua maswali sita yanayochangia kustawi kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (al.6)

7. a)Tofautisha kati ya uwili lugha na wingi lugha. (alama 4)

b)Taja sababu sita zinazosababisha watu kubadili na kuchanganya ndimi. (alama 6)

8. a)Eleza mambo yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya uhuru

(b)Eleza sifa tano za lugha rasmi.

9. (a) Eleza sababu tano zinazomfanya mtu kufanya makosa ya matamshi na sarufi katika mazungumzo yake.(al5)

(b) Eleza sababu tano zinazowafanya vijana kupenda kutumia misimu katika mawasiliano yao. (alama 5)

10. a)Eleza maana ya lugha ya taifa. (alama2)

b)Eleza majukumu manne ya Kiswahili nchini Kenya kama lugha ya taifa. (alama8)

11. Fafaua jinsi shughuli zifuatazo zitachangia kukua kwa lugha ya Kiswahili na kufaikisha ajenda ya amani na maridhiano nchini Kenya.

i) Vyombo vya habari na mawasiliano. alama 2)

ii) Uchapishaji (alama 2)

iii)Dini (alama 2)

iv)Siasa (alama 2)

v) Sanaa na maonyesho ya muziki. (alama 2)

12.

a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano ala 5)

b) ……..Sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa

i. Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili ala 1)

ii. Eleza sifa nne za sajili hiyo ala 4)

13.

MHUSIKA 1: Nidhamu , Mheshimiwa Sudi. Hili ni onyo dhidi ya tabia hiyo.

MHUSIKA II: Nisamehe Bwana……

MHUSIKA I: sasa ninakaribisha swali la tatu. Mheshimiwa Mambo, uliza swali lako.

MHUSIKA III: Ninaomba kufahamishwa ni kwa nini Waziri wa Maji ameshindwa kusambaza huduma za maji katika kijiji cha Walalahoi.

Maswali

a) Bainisha sajili ya makala haya. (al. 2)

b) Fafanua sifa za sajili hii. (al. 8)

14. Hujambo bwana: You look familiar, have we ever met before.... Sijui nilikuona wapi?

a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mifano mitatu kwenye makala. alama 2)

b) Fafanua sifa nyingine nne za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. (Alama 4)

c) Kwa kutumia mifano mwafaka eleza kaida nne za matumizi ya lugha. (Alama 4)

15. ***Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

A: Jina?

B: Ouma James

A: Umri?

B: Miaka ishirini

A: Una shida gani

B: Ninaendesha sana. Pia kichwa chaniwanga ajabu. (Anatiririkwa na machozi)

C: Anachukua stethoskopu na kumpima) Utapata nafuu hivi karibui ukinywa dawa nitakazokupa.

Maswali

a) Tambua rejesta inayorejelewa na Makala haya. (al 2)

b) Fafanua vitabulishi vine vinavyohusishwa na rejesta hiyo. (al 8)

16. (a) Eleza istilahi zifuatazo (Alama 4)

i) lugha

ii) misimu

(b) Andika sifa zozote sita za lugha utakayotumia kuwatangazia watu kinyang'anyiro cha soka. (Alama 6)

17. "....watu wa kaunti ya makueni wamesahaulika kabisa. Ningependa kuelezwa kinagaubaga kama hawa ni wakaenya au la. Order! Order! Mheshimiwa Tata.

La! Tumekuwa marginalized kwa muda mrefu sana.....

(i) Hii ni sajili gani? (Alama 2)

(ii) Eleza sifa nne za sajili iliyotajwa. (Alama8)

18.

a) Taja na ufafanue nadharia tatu zinazoelezea asili ya lugha ya Kiswahili (alama 6)

b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimujamii

(i) Lafudhi (Alama 2)

(ii) Rejesta (Alama 2)

19. Eleza sifa zozote tano za lugha ya siasa (alama 10)

20.

a) Eleza maana ya sajili. (alama 2)

b) Fafanua umuhimu wa sajili katika jamii. (alama 10)

21. ***Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Mwatani: Rusha hiyo ball haraka tumechelewa five minutes. Twende daro.

Omoshi: Harakisha mode anacome.

Bwana Kipiti: Nendeni darasani haraka! Kisha kiranja awape vitabu vyenu vya insha ili mwandike barua.

Mwatani: Sawa mwalimu. Samahani kwa kuchelewa uwanjani.

Omoshi: Je, tutaandika barua rasmi au barua ya kawaida?

Bwana Kipiti: Mwandike barua rasmi. Je, mnakumbuka muundo wake?

Omoshi na Mwatani: Ndio mwalimu. Ulitufundisha jana. Asante sana mwalimu.

Bwana Kipiti: Kumbukeni idadi ya maneno. Idadi ya maneno ni muhimu katika uandishi wa insha.

Maswali

a) Eleza sajili katika dondoo. (alama 2)

b) (Eleza sifa nane za sajili hii zinazopatikana katika dondoo. (alama 8)

22. i) Eleza maana ya lakabu. (alama 1)

(ii) Eleza dhima ya lakabu katika jamii. (alama 4)

23 a) Eleza mitazamo mine kuhusu chimbuko la Kiswahili. (alama 4

b)Eleza njia za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. (alama 6)

24. (a) Ali: Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!

25. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

Maswali

(i) Weka maneno haya katika sajili yake. (alama 2)

(ii) Nini kimekufanya uchague sajili uliochagua katika swali (i). (alama 1)

(iii) Eleza sifa za matumizi lugha katika sajili hii. (alama 7)

26. a) Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili. alama6)

b) Fafanua istilahi zifuatazo: (alama 4)

i. UwiliLugha

ii. LinguaFranka

iii. Misimu

iv. Sajili

27. (a) (i) Eleza maana ya krioli. (alama 2)

(ii) Eleza sifa zozote tatu za krioli. (alama 3)

(b) (i) Eleza maana ya Lingua Franka (alama 2)

(ii) Tambua sifa zozote tatu za Lingua Franka (alama 3)

28.

a) Eleza majukumu **matatu** ya lugha ya taifa. (alama 3)

b) Fafanua mtindo wa lugha uliotumiwa katika taarifa ifuatayo huku ukieleza sababu za matumizi ya vitambulisho maalum vya lugha. (alama 4)

Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa. Sina la kusema, ila ninawakumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi ya taifa zima. Mtu huyo ni mimi na ninajitahidi niwezavyo kujenga masoko, barabara, shule zaidi na mazahanati na maisha yenu yatakuwa ya raha zaidi.

c) Thibtisha kuwa adabu za lugha hazizingatiwi miongoni mwa wanajamii siku hizi. (alama 3)

29. a) Eleza sababu zozote sita zinazochangia kufa kwa lugha. (alama 6)

b) Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili (alama4)

31. Eleza makosa matano yanayoweza kutokea wakati wa mazungumzo. (alama 10)

MTIHANI 10

USHAIRI WA 1

Soma shairi lifuatalo kwa makini halafu ujibu maswali yanayofuata

1. Naja sasa ni ndiyani, naja kwetu Mzalendo
   Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando
   Kwetu' mi nakutamani, kulo na mwingi uhondo
   Nijaye ni yule nyundo, misumari hadharini

2. Naja kwingine kuwapi, kulojaa langu pendo?
   Huenda nende kwinginepi, sawa nako kwa muundo?
   Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando?
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

3. Naja nije rudi papo, panigedeme mgando
   Ningaambwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo
   Sitakwenda penginepo, tarudi kuko kwa mwando
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

4. Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna vimondo
   'Takuja kuvilekeya, vinganijiya kwa vundo
   nilipozawa tafiya, sikimbii kwenda kando
   nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

5. Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivyo mwando
   Tena n'najiandaa, kwa fikira na vitendo
   Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

6. Naja na ingawa naja, siwaeki mifundo
   Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendwa mwando
   Ela wataoningoja, na vyao viwi vitendo
   Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

Maswali

7. a) Eleza jinsi 'uzalendo' wa mshairi unavyojitokeza katika beti za 1 na 2 alama 4
   b) Fafanua jazanda zinazopatikana katika mshororo:
      Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando? alama 2
   c) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari alama 4
   d) (i) Katika ubeti wa 5 mshairi amebadilika Eleza alama 2
      (ii) Ananuia kufanya nini pindi arudipo? Alama 2
   e) Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa 6 alama 2
   f) Andika maneno haya katika kiswahili sanifu alama 2
      a. Mwando
      b. Ningambwa
   g) Kibwagizo cha shairi kinampa sifa gani mshairi? Alama 2

USHAIRI WA 2

Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Jukwani naingia, huku hapa pasokota,
Kwa uchungu ninalia,hii tumbo nitaikata,
Msiba mejiletea,nimekila kiso takata,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Wazee hata vijana,wote umewasubua,
Huruma nao hauna,heshima kawakosea,
Ukambani na Sagana,hata mbwa wararua,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Wahasibu ofisini,kibwebwe mejifunga,
Miaka mingi vitabuni,ili wasikose unga,
Nadhari wanadhamini,hesabu wanazirenga,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wapenzi wa kiholela,pia wanakuogopa,
Baada yao kulala, wana wao wanatupa,
Wakihitaji chakula,wanachokora mapipa,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Wafugaji hata nao,kama dawa wakwamini,
Hawajali jiranio,wamesusia amani,
Wanaiba ng'ombe wao,na kuzua kisirani,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Nayo mizozo ya maji, kaonekana kwa mara,
Hiyo nayo ni dibaji,sababu sio harara,
Njaa wahepe wenyeji, huo ndio mkarara,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Ningeweza kukuuza,ingekuwa siku njema,
Tena kwa bei ya meza,sokoni nimesimama,
Wala tena singewaza,kuhusu wali na sima,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Hatima umefikika,naenda zangu nikale,
Mate yanidondoka,kwa mnukio wa wale,
Naomba kwenda kukaa,wala sio nikalale,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Maswali

i Lipe anwani mwafaka shairi hili. (Alama 2)
ii Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (Alama 2)
iii Huku ukitolea mifano mwafaka, taja arudhi zilizotumiwa katika ubeti wa tatu. (Alama 4)
iv Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (Alama 4)

v Thibitisha kuwepo kwa idhini ya ushairi. (Alama 2)
vi Taja madhila anayoelezea mtunzi wa shairi hili yaletwayo na tumbo. (Alama 4)
vii Elezea maana ya maneno yafuatayo. (a)dibaji (b) harara (Alama 2)

USHAIRI WA 3

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

LAU HAKUNA MAUTI. Na Abdalla Said Kizere

1. Lau dunia nanena, tuseme si ati ati,
Mauti kawa hakuna, katika wote wakati,
Vipi tungelisongana, tunaoishi tiati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

2. Dunia ingetatana, na kizazi katikati,
Huku kwazaliwa bwana, kule kwazawa binti,
Vipi tungelioana, na kuzaa hatuwati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

3. Lau mauti hakuna, tungesongana sharuti,
Kwa viumbe kukazana, wanadamu na manyati,
Vipi tungelijazana, kwa kusitawi umati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

4. Walakini Subuhana, kapanga sisi na miti,
Ili tusizidi sana, si wengi na si katiti
Maisha ya kupishana, yule ende yule keti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

5. Ndipo dunia kufana, ikawa kama yakuti,
Kwa uwezowe Rabana, kaipanga madhubuti,
Maisha kugawiana, kayagawa kwa mauti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

6. Njia ingekuwa hapana, pembeni na katikati,
Sote tungeambatana, kama ukosi na shati,
Na njaa ingetutafuna, pa kulima hatupati,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

7. Peleleza utaona, hayataki utafiti,
Kama tungelikongana, ingekuwa ni bahati,
Vipi tungesukumana, katika hiyo hayati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

8. Mbele sitokwenda tena, hapa mwisho nasukuti,
Yaoleni waungwana, shauri yake Jabaruti,
Yote tuloelezana, katenda bila senti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

MASWALI

a) Je, hili ni shairi la bahari gani? Eleza (alama 2)
b) Eleza vile mwandishi alivyotumia uhuru wa kishairi (alama 4)
c) Eleza umbo la shairi hili (alama 4)
d) Fafanua ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano (alama 4)
e) Andika majina mawili ya Mungu kwa mujibu wa shairi (alama 2)
f) Kwa kutolea mifano, eleza mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na shairi (alama 2)
(i) Tiati _____(ii) Shani_____

USHAIRI WA 4

Soma shairi lifuatalo, kisha ujibu maswali; (alama 20)
Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwendani,

Afiya yangu dhahili, mno nataka amani,
Nawe umenikabili, nenende sipitalini,
Sisi tokea azali, twenda zetu mizimuni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani,
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini,
Kwa nguvu za kirijali, mkuyati uamini,
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele Fulani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zongo huauni,
Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalondani,
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini,
Dakitari k'ona mwili, tanena kensa tumboni,
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni,
Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani,
Wambiwa damu kalili, ndugu msaidieni,
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo buriani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu thamani,
Ulete kuku wawili, wa manjano na kijani,
Matunda pia asali, vitu vyae chanoni,
Nafwatani sipitali, na dawa zi mlangoni?

MASWALI

a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)
b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili? (alama 2)
c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitali? (alama 4)
d) Kwa kuzingatia muundo wa shairi hili, eleza mbinu zilizotumika (alama 6)
e) kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi? (alama 2)
f) **Andika maana ya maneno yafuatayo yalivyotumika katika shairi** (alama 4)
i) Dhahili ii) Azali iii) Sahali iv) Tumbo nyangwe

USHAIRI WA 5

1. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali.

Niokoa Muokozi, uniondolee mashaka.
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekithiri simanzi, ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo.

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua
Naomba hisikitika, na mikono hiinua
Mtenda ndiwe Moliwa, nipate niyatakayo.

Mtenda ndiwe Moliwa, we ndiwe Mola wa anga
Mazito kuyaondoa, pamoja na kuyatenga
Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilonifunga
Nikundulia muwanga, nipate niyatakayo

Muwanga nikundulia, nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea, itoke mwangu moyoni
Mambo mema niegheshea, maovu nisitamani.
Nitendea we Manani, nipate niyatakayo.

Igeuze yangu nia, dhaifu unipe mema
Nili katika dunia, kwa afia na uzima
Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema
Nifurahike mtima, nipate niyatakayo.

MASWALI

(a) Shairi hili ni la bahari gani? Eleza. (alama 2)
(b) Taja madhumuni ya shairi hili. (alama 3)
(c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
(d) Thibitisha namna uhuru wa kishairi unaibuka katika shairi. (alama 4)
(e) Andika ubeti wa pili katika lugha sufufu. (alama 4)
(f) Toa maana ya:
(i)Nimedhikika(ii) Muwanga nikundulia (iii)Nifurahike mtima(alama 3)

Kwa majibu ya maswali haya piga simu ama utume ujumbe kwa

BWANA CHEPKWONY COSMAS **0724351706** ulipie 250/- upate usaidizi